**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**MKOA WA SIMIYU,**
**Simu Na: 0753 321 860**
**Baruapepe: info@simiyurrh.go.tz**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA,**
**S.L.P 17,**
**BARIADI - SIMIYU**

Kumb Na: SIMRR/S.06/36

31/08/2023

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA KUJITOLEA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, inatangaza nafasi za ajira za kujitolea kwa kada Mbalimbali kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) kama ifuatavyo;

| NA | KADA | NAFASI |
|---|---|---|
| 1 | Wauguzi Daraja la II (Enrolled Nurse) | 4 |
| 2 | Dereva | 1 |
| 3 | Mortuary Attendant (Mhudumu wa Chumba cha kuhifadhi Maiti | 1 |
| 4 | Wasaidizi wa Afya | 6 |

A. **WAUGUZI DARAJA LA II – TGHS A NAFASI 4**

**a) Sifa za muombaji.**

Awe wenye cheti cha uuguzi cha miaka miwili kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na baraza la wauguzi na wakunga Tanzania.

**b) Kazi na majukumu.**

i. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
ii. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi.
iii. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi.
iv. Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
v. Kutoa ushauri nasaha.
vi. Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango.
vii. Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto.
viii. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya.
ix. Kufuatilia utendaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi.

x. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

B. **DEREVA**

**a) Mwombaji anatakiwa awe na Sifa zifuatazo;**

i. Awe amehitimu kidato cha nne (IV) au cha sita (VI) na kufaulu
ii. Awe na leseni Daraja la C au E, ya uendeshaji wa magari, ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja.
iii. Asiwe mwajiriwa wa Serikali.
iv. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course). yanayotolewa na NIT, Veta au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.
v. Mwombaji awe na cheti cha majaribio ya ufundi Daraja II (Trade Grade II)
vi. Kila mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho wa Taifa (NIDA).
vii. Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili na watakaoshindwa kuzingatia masharti ya tangazo hili hawataitwa.
viii. Waombaji waambatishe wasifu wa mwombaji (CV), akionesha namba za simu na anwani yake na wadhamini watatu (3) wa uhakika, vyeti vya elimu na taaluma.
ix. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua mwaka mmoja katika taaluma hiyo akiwa anafanya kazi, hivyo waombaji wenye uzoefu wa muda mrefu watapewa kipaumbele.

**b) Kazi**

i. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
ii. Kutunza na kuaandaa Daftari la safari "Log Book" kwa safari zote.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za Udereva.

v. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali kwa kuzingatia maelekezo utakayopewa na Msimamizi wako wa kazi.

vi. Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na mwajiri wako.

C. **MHUDUMU WA CHUMBA CHA MAITI- TGHOS A NAFASI-1**

a) **Sifa za mwombaji.**

Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne na kupata mafunzo ya kudumu katika chumba cha maiti(Mortuary attendant).

b) **Kazi na majukumu.**

i. Kufanya usafi wa chumba cha kuhifadhia maiti.

ii. Kupokea, Kuosha na Kutunza maiti.

iii. Kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

D. **MHUDUMU WA AFYA- TGHOS A NAFASI 6.**

a) **Sifa za mwombaji.**

Awe amehitimu kidato cha nne waliopata mafunzo ya mwaka mmoja katika mafunzo ya afya.

b) **Kazi na majukumu.**

i. Kufanya usafi wa vifaa vya kazi, usafi wa wodi, na mazingira.

ii. Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza katika kwenda haja (Kubwa na ndogo) na kuoga.

iii. Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiejiweza.

iv. Kuchukua nguo za mgonjwa kuzipeleka kwenda kufuliwa.

v. Kuchukua sampuli za mgonjwa kwa ajili ya vipimo vya maabara na kufuatilia majibu.

vi. Kutayalisha vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufunga majeraha.

vii. Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa.

viii. Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

c) **MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI.**

Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa za jumla kama ifuatavyo

i. Awe Raia wa Tanzania.

ii. Awe na umri usiozidi miaka 45.

iii. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea (Cheti cha kidato cha Nne, Sita, Taaluma na Usajili kamili) "Full Registration" au Leseni hai ya kufanya kazi ya taaluma husika.
iv. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la Jinai au kufungwa jela.
v. Maombi yaambatane na wasifu wa mwombaji (CV).
vi. Maombi yaambatishwe na nakala ya vyeti vya Elimu, Taaluma na Cheti cha Kuzaliwa.
vii. Testimonials Results Slips **HAZITAKUBALIWA**.

**Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 14/09/2023**

Maombi yatumwe kwa;

Mganga Mfawidhi,

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Simiyu,

S.L.P 17,

**BARIADI-SIMIYU.**

Au tuma kwa barua pepe: info@simiyurrh.go.tz

Imetolewa na;

..............................................

**Dkt. Athanas Ngambakubi**

**MGANGA MFAWIDHI**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SIMIYU**

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA
YA MKOA - SIMIYU